


**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EANSO
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya.

*Tim Mwenesi Mugesani[1], Dr. Juliet Akinyi Jagero, PhD[1] & Dr. Naomi Nzilani Musembi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknologia cha Jaramogi Oginga Odinga, S. L. P. 210-40601, Bondo, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0002-8032-9310; Barua pepe ya mawasiliano: Mwenesi215@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*08 Machi 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Lugha Ya Msimu, Umaratokezi, Upokezilugha, Kiingizi Cha Kiisimu.*

**IKISIRI**

Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha iliyopangwa kisera kufundishwa kama somo la lazima kuanzia kiwango cha awali cha elimu ya shule za msingi nchini Kenya hasa katika mji wa Mbale ambao ndio mji mkuu wa Jimbo la Vihiga. Hata hivyo, kuwepo kwa matumizi ya lugha ya msimu ya Sheng miongoni mwa vijana wa mijini kumesababisha utata katika ufundishaji wa msimbo rasmi wa Kiswahili. Wanadaraja la awali katika shule za msingi hususan zile zinazopatikana mjini Mbale huenda wakaitumia lugha ya msimu ya Sheng katika mawasiliano yao wawapo shuleni. Hali hii inaweza kutatiza upokezilugha wa Kiswahili. Madhumuni ya makala hii ni kutathmini umaratokezi wa msamiati maarufu wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Msingi wa Matumizi iliyoasisiwa na Tomasello (2003). Data katika utafiti huu ilitokana na utafiti wa nyanjani. Mbinu ya uchunzaji ilitumika katika kukusanya data hususan kwa kutumia mwongozo wa uchunzaji. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba umaratokezi wa juu wa kiingizi cha kiisimu huweza kuchangia katika upokezilugha. Matokeo yanadhihirisha kuwa umaratokezi wa juu wa msamiati maarufu wa Sheng unawezesha upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali. Makala hii ni muhimu kwa vile inadhihirisha mbinu bora ambayo inaweza kutumiwa kushirikisha msamiati maarufu wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

**APA CITATION**

Mugesani, T. M., Jagero, J. A., & Musembi, N. N. (2022). Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 39-48. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578.

**CHICAGO CITATION**

Mugesani, Tim Mwenesi, Juliet Akinyi Jagero & Naomi Nzilani Musembi. 2022. "Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 39-48. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578.

**HARVARD CITATION**

Mugesani, T. M., Jagero, J. A., & Musembi N. N. (2022) "Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 39-48. doi: 10.37284/jammk.5.1.578.

**IEEE CITATION**

T. M. Mugesani, J. A. Jagero, & N. N. Musembi, "Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 39-48, Mar. 2022.

**MLA CITATION**

Mugesani, Tim Mwenesi, Juliet Akinyi Jagero & Naomi Nzilani Musembi. "Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Upokezilugha wa Kiswahili Miongoni mwa Wanadaraja la Awali Katika Shule za Msingi Mjini Mbale, Kaunti ya Vihiga, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Mar. 2022, pp. 39-48, doi:10.37284/jammk.5.1.578.

## UTANGULIZI

Matumizi ya lugha ya msimu ya Sheng nchini Kenya hasa kwa ajili ya mawasiliano miongoni mwa vijana wa mijini yanaendelea kuimarika kila siku. Sheng imewasilisha hali tata hususan matumizi yake yanapodhihirika katika mazingira ya shule ambako haitambuliwi na sera yoyote kama lugha ya mawasiliano wala ya kufundishia. Tafiti mbalimbali zimekwisha kufanywa kuhusiana na Sheng. Jambo linalojitokeza kwa baadhi ya matokeo ya tafiti hizo ni kwamba Sheng ina athari hasi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Pengine, matumizi ya Sheng yameonekana kuwa na athari chanya kwani inaonekana kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watumizi wake ambao wengi wao ni vijana. Vilevile imebainika kuwa siku hizi mbali na vijana, Sheng hutumiwa hata na watoto, watu wa umri wa makamo na wazee. Kuna baadhi ya waandishi maarufu ambao wamekwisha shirikisha msamiati wa Sheng katika uandishi wao. Vyombo vya habari kama vile runinga, redio na mitandao ya kijamii pia havijaachwa nyuma katika matumizi ya Sheng aidha katika vipindi maarufu ama katika matangazo ya biashara. Hizi ni baadhi ya mbinu ambazo zinaendelea kuchangia pakubwa katika kueneza matumizi ya Sheng nchini Kenya vivyo hivyo kuifanya kuwa maarufu.

Matumizi ya Sheng yamepuuzwa na sera ya lugha ya kufundishia kwa sababu Sheng inachanganya miundo ya kiisimu ya Kiswahili, Kiingereza na lugha za kienyeji za Kiafrika katika miji ya nchini Kenya hususan mji wa Mbale. Kwa hivyo haikubaliki kwani inaweza kutatiza umilisi wa msimbo rasmi ambao ni Kiswahili.

Mbinu mbalimbali zinazohusiana na uundaji wa maneno ya Sheng pamoja na miktadha ya matumizi yake zimeonyesha kwamba Sheng hutumia mbinu bia za uundaji maneno namna ilivyo katika lugha kuu zinazotambulika kama vile Kiswahili na Kiingereza. Mifano ya mbinu hizo ni ubunaji kinasibu, ukopaji, utohozi, ufupishaji, ubadilishaji silabi, uambatishaji na nyenginezo (Ogechi, 2005). Kwa hivyo wasomi na watafiti wengi wa Sheng wanakubaliana kwamba muundo wa msamiati wa Sheng ni sawa na ule wa sarufi ya Kiswahili ingawa haieleweki ni kwa nini Sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake (Kitula na Kobia, 2000).

Githinji (2013) anaeleza kwamba Sheng inafaa kutambuliwa na nafasi yake kubainishwa katika sera ya lugha ya taifa. Sheng inaweza kuchangia sana katika usanifishaji wa Kiswahili, hasa katika upande wa uundaji wa msamiati. Mji wa Mbale ndio mji mkuu wa jimbo la Vihiga, Kenya. Mjini humo mnapatikana shule za msingi za umma na za

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

kibinafsi. Ijapokuwa Sheng ni lugha ya msimu, hutumiwa katika mawasiliano pamoja na lugha kama vile Kimaragoli, Kiswahili, Kiingereza, Kidholuo na nyinginezo kutoka jamiilugha mbalimbali za Kenya. Licha ya kutumiwa kimawasiliano mjini Mbale, Sheng haitambuliwi na sera ya lugha ya kufundishia shuleni wala kama lugha ya mawasiliano katika shughuli za jamii ya mji wa Mbale. Madhumuni ya makala hii ni kuonyesha umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali katika shule za msingi mjini Mbale.

Upokezilugha ni utaratibu ambao humwezesha mtoto kunasa na kuvifahamu polepole vipengele mbalimbali vya lugha. Utafiti ulidhamiria kuonyesha namna umaratokezi wa msamiati wa Sheng unavyowezesha mchakato wa upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali. Hii ni kwa sababu, wanadaraja la awali wako katika kiwango cha umri mchanga. Umri huu ndio muhimu hasa kwa mtoto kupokea lugha kwa ajili ya mawasiliano.

## MSINGI WA NADHARIA KUHUSU UPOKEZILUGHA

Nadharia ya Msingi wa Matumizi iliyoasisiwa na Tomasello (2003) iliongoza utafiti huu. Nadharia hii inashikilia kwamba, mfumo wa kiisimu umo ndani mwa mazungumzo ya kiuamilifu; yaani muundo wa kiisimu huibuka kutokana na uzoefu wa matumizi ya lugha (Langacker, 1987; Tomasello, 2003). Nadharia ya Msingi wa Matumizi ina mihimili mikuu miwili katika isimu mawasiliano. Mhimili wa kwanza ni ule wa maana ni matumizi. Mhimili wa pili ni ule wa muundo wa kiisimu huibuka kutoka kwa matumizi. Nadharia ya Msingi wa Matumizi ilifaidi utafiti kwa sababu ina uwezo wa kutoa mwelekeo wa kuchunguza upokezilugha miongoni mwa wanafunzi wanaopokea kiingizi cha lugha katika kiwango cha chini. Vilevile huchunguza uhusiano kati ya ruwaza za kiingizi na athari ya lugha ya msimu katika upokezilugha. Kulingana na mawazo ya Nadharia ya Msingi wa Matumizi, lugha ya msimu ya Sheng inaonekana kuwakilisha kiingizi cha upokezilugha wa Kiswahili katika kiwango cha chini. Mawazo haya yanakubaliana na mengine kwamba kiingizi kilicho na thamani kubwa katika upokezilugha ni ile lugha ambayo imepiga hatua zaidi katika miundo ambayo mwanafunzi wa lugha tayari amepokea (Krashen, 1981).

Mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi ndiyo uliokuwa muhimu kutathmini umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali. Mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi unashirikisha dhana ya uundaji skima. Katika uundaji wa skima, huwa inachunguzwa namna watoto hujenga miundo dhahania ya kisintaksia kutoka kwa mazungumzo ambayo wamekwishakusikia. Skima ni muundo wa kisemantiki, fonolojia au ishara ambao kwa kuhusiana na kiwakilishi kingine cha kipashio sawa, huwa na sifa maalumu na habari chache (Langacker, 1987).

Ushahidi uko kwamba hata watoto wachanga wanajua kutambua vizuri ruwaza za skima na udhahanishaji wake. Hii ina maana kwamba umilisi wa kiisimu ni tokeo la matumizi ya lugha (Tomasello, 2003). Jambo hili lilikuwa muhimu kwa utafiti kwa kuwa wango la utafiti lilikuwa wanadaraja la awali ambao wako katika kikundi cha umri mchanga. Umri mchanga ndiyo unaoaminiwa kuwa muhimu katika upokezilugha hasa wa lugha kama vile Kiswahili.

Uundaji wa skima huweza kutokana na aina ya umaratokezi. Umaratokezi unahusu umbo la kiisimu kujitokeza mara nyingi katika kiingizi cha kiisimu. Kwa hivyo, kutokana na mazoea haya, uwakilishi wa kiingizi cha kiisimu huimarika kwa mtoto na hili humfanya kulitoa umbo la kiisimu kwa urahisi anapohitaji kulitumia katika mawasiliano wakati mwingine (Saxton, 2010). Umaratokezi wa juu kiishara husababisha udhibiti na uhifadhi wa kiwango kizima cha kiisimu. Isitoshe, umaratokezi wa juu kiishara huongeza umahiri wa lugha na kuimarisha uwakilishi wa kumbukizi. Umaratokezi wa kiishara katika miandamano ukiwa wa kiwango cha juu, basi kuna uwezekano kwamba ishara za kiisimu zitahifadhiwa na kutolewa zote (Tomasello, 2003).

Aina ya umaratokezi husaidia katika utambuzi wa mlingano kati ya miundo, kwa hivyo huhitajika ili kuweka wazi miundo ya maneno na virai. Pia aina ya umaratokezi wa juu huupa muundo uwezo mkubwa wa kuwakilishwa, hivyo kuufanya uwepo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

au utolewe kwa matumizi muhimu (Bybee, 2006). Skima huchangia katika upokezilugha kwa sababu kategoria za skima ya juu huweza kupelekwa kwa urahisi hadi kwa faridi mpya. Kwa hivyo, skima huchangia katika kuunda kategoria za kiisimu.

Mawazo yanayotokana na uundaji skima yalikuwa muhimu katika kuonyesha namna msamiati maarufu wa Sheng unawezesha uundaji wa skima ya juu au ya chini katika upokezilugha wa Kiswahili. Iwapo skima ingekuwa ya chini, basi kiingizi cha kiisimu katika upokezilugha wa Kiswahili huenda kingekuwa cha chini, kinyume na iwapo skima iliyoundwa ingekuwa ya juu.

Umaratokezi wa miundo ya Sheng kwenye kiingizi cha lugha ya Kiswahili ulifaa kwa ajili ya kutathmini umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale.

## NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

Utafiti ulichukua muundo wa usanifu muhula. Mbinu ya kukusanya data ya utafiti ilikuwa uchunzaji wa kipindi cha Kiswahili darasani ambao ulishirikisha wanadaraja la awali katika shule za msingi mjini Mbale. Mbinu hii ilitumika kukusanya data ya matamshi ya maneno ya wanadaraja la awali katika shule za msingi mjini Mbale. Kwa mujibu wa Tomasello na Stahl (2004), data ya aina hii huwa faafu na ya kina mno wakati wa kuchunguza muktadha wa upokezilugha. Isitoshe, huwa muhimu katika uchunguzi wa ruwaza za jumla katika maendeleo ya lugha. Isitoshe, mbinu ya uchunzaji mara nyingi hutumika katika muktadha wa darasa ili kutazama kiwango ambacho mwanafunzi wa upokezilugha hutumia mikakati ya kutafuta mbinu mbadala ya kusema jambo ambalo hajui namna ya kusema (Macaro, 2001). Mbinu hii ilikuwa muhimu katika kutathmini umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale.

### Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ya utafiti iliteuliwa kimakusudi. Usampulishaji wa kimakusudi ni utaratibu usiokadiria uwezekano kwamba kila faridi katika wango la utafiti itahusishwa kwenye sampuli. Badala yake, sampuli huteuliwa kimakusudi kwa msingi kuwa wango ndogo la utafiti linaloteuliwa kutoka kwa lile kubwa litawakilisha wango nzima la utafiti (Kothari, 2004). Mji wa Mbale uliteuliwa kimakusudi kwa sababu uliafiki sifa kuu ya wango la utafiti ambayo ni wanadaraja la awali walio katika umri mchanga. Umri huu ndiyo muhimu katika mchakato wa upokezilugha bora wa Kiswahili. Mji wa Mbale una shule saba za msingi ambapo tano ni za umma huku mbili zikiwa za binafsi. Shule nne ziliteuliwa kimakusudi kutegemea eneo zinakopatikana mjini Mbale na umiliki; tatu zilikuwa za umma na moja ya kibinafsi.

Usampulishaji nasibu ulitumika kuchagua darasa moja moja kwa dhamira ya uchunzaji wa kipindi cha Kiswahili. Hii ilihusu kuteua sampuli kwa namna ambayo hakuna yeyote katika wango la jumla angeweza kupata nafasi zaidi ya kuchaguliwa kushinda mwingine.

### Uchanganuzi wa Data

Data ya utafiti ilitokana na uchunzaji wa kipindi cha Kiswahili darasani. Data ilichanganuliwa kiufafanuzi na kitakwimu kuambatana na madhumuni ya utafiti na vipengele vya nadharia ya Msingi wa Matumizi (Tomasello, 2003). Mwelekeo wa Msingi wa Matumizi hujikita katika kueleza maendeleo ya ruwaza za matumizi zinazojitokeza kwenye data. Vilevile hueleza uwezekano wa kuwepo kwa uhusiano wa hizo ruwaza na kiingizi cha lugha kilichopokewa.

Uchanganuzi wa data kiufafanuzi ulinuiwa kutoa maelezo ya namna msamiati wa Sheng ulio na umaratokezi wa juu unawezesha upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale. Uchanganuzi kitakwimu ulitoa fursa ya kuonyesha idadi ya ishara za kiisimu kwa lengo la kutathmini umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng

Data kuhusiana na umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale ilipatikana kutokana na uchunzaji wa kipindi cha Kiswahili darasani.

Mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi katika nadharia ya Msingi wa Matumizi uliongoza katika kueleza umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili. Mhimili huu uliwasilisha kipengele cha uundaji skima ambacho hutokana na aina ya umaratokezi. Umaratokezi unahusu umbo la kiisimu kujitokeza mara nyingi katika kiingizi cha upokezilugha (Tomasello, 2003).

Matokeo ya umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng yameonyeshwa katika majedwali mbalimbali kwa kurejelea kila shule iliyoshiriki utafiti. Hata hivyo, ufafanuzi wa matokeo umejikita tu katika msamiati teule wa Sheng ambao ulitokea zaidi ya mara moja katika matamshi kuambatana na mwongozo wa uchunzaji miongoni mwa wanadaraja la awali. Uamuzi huu unaegemea mawazo ya mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi ambao unaeleza kuwa, kutokana na urudiaji wa matumizi ya kipashio cha kiisimu, mzungumzaji huanza kutambua ruwaza zinazohusika na vipashio maalum vya kiisimu (Lieven na Tomasello, 2008; Tomasello, 2003).

**Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Shule ya Hambale**

Matokeo ya umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng jinsi ulivyotumika darasani miongoni mwa wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Hambale yamewasilishwa katika *Jedwali 1* lifuatalo:

**Jedwali 1: Umaratokezi wa Msamiati wa Sheng Katika Shule ya Hambale**

| **Sheng** | **Shule** | **Hambale** | | | **Jumla** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasa** | **1** | **2** | **3** | | |
| | **Kiswahili** | | | | | |
| *Ticha* | Mwalimu | 06 | 07 | 07 | 20 | 60.607 |
| *Mtoi* | Mtoto | 03 | - | - | 03 | 9.091 |
| *Susuu* | Enda haja ndogo | 03 | - | - | 03 | 9.091 |
| *Moti* | Motokaa | - | 01 | 01 | 02 | 6.061 |
| *Tao* | Mjini | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| *Piko* | Pikipiki | - | - | 01 | 01 | 3.030 |
| *Poa* | Vizuri | 01 | - | - | 01 | 3.030 |
| *Kanjo* | Askari wa baraza la mji | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| *Soo* | Shilingi mia moja | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| Jumla | | 13 | 11 | 09 | 33 | |
| % | | 39.394 | 33.333 | 27.273 | | 100 |

Maneno tisa ya Sheng kutokana na idadi jumla ya maneno kumi na tano yaliyokuwa kwenye mwongozo wa uchunzaji yalibainika katika matumizi ya wanadaraja la awali wakati wa somo la Kiswahili katika Shule ya Msingi ya Hambale.

Kwa mujibu wa maelezo ya mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi katika Nadharia ya Msingi wa Matumizi, marafukizi ya kiishara katika miandamano ikiwa juu, basi kuna uwezekano wa kuhifadhiwa na kutolewa kwa uzima. Utafiti ulionyesha mifano ya msamiati wa Sheng ambao ulidhihirisha skima ya juu kwa mujibu wa Jedwali 1 ni maneno *ticha*, *mtoi*, *susuu* na *moti*.

Kulingana na Jedwali 1, neno *ticha* lilikuwa na idadi ya asilimia 60.607 ya umaratokezi miongoni mwa wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Hambale. Maneno *mtoi* na *susuu* yalikuwa na umaratokezi wa kiwango sawa cha asilimia 9.091. Neno *moti* ambalo muundo wake kwa Kiswahili Sanifu ni motokaa kutokana na utohozi wa neno la Kiingereza ‘‘*motor vehicle*,’’ lilikuwa na umaratokezi wa asilimia 6.061.

Vilevile kulingana na Jedwali 1, maneno yafuatayo yameonyeshwa kwa asilimia inayolingana ya 3.03 kila moja: *tao* ambalo limetokana na utohozi wa neno la Kiingereza “*town*” na ambalo kwa Kiswahili linamaanisha mji; neno *piko* ambalo kwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

Kiswahili Sanifu ni pikipiki; neno *poa* ambalo kwa Kiswahili Sanifu humaanisha vizuri; neno *kanjo* ambalo ni utohozi wa neno la Kiingereza "*council*" na kwa Kiswahili Sanifu linamaanisha baraza lakini hapa muundo wake umepewa maana ya askari wa baraza la mji; neno *soo* pia lilijitokeza nalo lilitumika kwa maana ya shilingi mia moja. Matokeo ya utafiti yanaafikiana na hoja ya Ogechi (2005) katika utafiti wake uliohusu mbinu za uundaji wa maneno ya Sheng, anaeleza kwamba mojawapo wa njia zinazotumika katika kuunda msamiati wa Sheng ni utohozi. Mifano kulingana na Jedwali 1 ni neno *ticha*, *moti*, *tao* na *kanjo* ambayo yametoholewa kutoka lugha ya Kiingereza. Maneno mengine kama vile *mtoi* na *piko* yametokana na mbinu ya ufupishaji. Hata hivyo, utafiti wake haukuonyesha umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika upokezilugha. Utafiti huu uliazimia kujaza mwanya huo wa kitaaluma kwa kuonyesha namna umaratokezi wa msamiati wa Sheng unaweza kuchangia katika upokezi wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali.

Jedwali 1 pia linaonyesha kwamba, idadi ya asilimia 39.394 ya wanafunzi wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi ya Hambale ilikuwa na umaratokezi wa juu wa matumizi ya msamiati teule wa Sheng ikilinganishwa na idadi ya asilimia 33.333 ya wanafunzi wa darasa la pili na idadi ya asilimia 27.273 ya wanafunzi wa darasa la tatu.

Matokeo ya utafiti yanathibitisha kuwepo kwa mfanano wa matumizi katika miundo ya msamiati wa Sheng na ya Kiswahili. Kwa mfano, wanadaraja la awali walitumia neno la Sheng *ticha* kwa kufananisha na neno la Kiswahili mwalimu, neno *mtoi* kufananishwa na mtoto (Kiswahili), *susuu* lililinganishwa na kuenda haja ndogo (Kiswahili) na neno *moti* lililinganishwa na motokaa au gari (Kiswahili).

**Umaratokezi katika Shule ya Mukuli**

Umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng miongoni mwa wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Mukuli ulitokana na uchunzaji wa somo la Kiswahili darasani. Matokeo yamewasilishwa katika *Jedwali 2* ifuatavyo:

**Jedwali 2: Umaratokezi katika Shule ya Mukuli**

| **Sheng** | **Shule** | **Mukuli** | | | **Jumla** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasa** | **1** | **2** | **3** | | |
| | **Kiswahili** | | | | | |
| *Ticha* | Mwalimu | 05 | 06 | 11 | 22 | 66.667 |
| *Mtoi* | Mtoto | 05 | - | - | 05 | 15.152 |
| *Piko* | Pikipiki | 02 | - | - | 02 | 6.061 |
| *Poa* | Vizuri | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| *Susuu* | Enda haja ndogo | 01 | - | - | 01 | 3.030 |
| *Sonko* | Tajiri | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| *Bamba* | Furahisha | - | 01 | - | 01 | 3.030 |
| Jumla | | 13 | 09 | 11 | 33 | |
| % | | 39.394 | 27.273 | 33.333 | | 100 |

Maneno saba kati ya kumi na tano yaliyokuwa kwenye mwongozo wa uchunzaji yalitumiwa na wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Mukuli.

Kulingana na *Jedwali 2,* neno *ticha* lilitamkwa na wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Mukuli kwa umaratokezi wa asilimia 66.667. Hili lilifuatiwa na neno *mtoi* ambalo lilitamkwa kwa umaratokezi wa asilimia 15.152; neno *piko* lilitamkwa kwa umaratokezi wa asilimia 6.061.

Kulingana na *Jedwali 2*, maneno *poa*, *susuu*, *sonko* na *bamba* yalikuwa na umaratokezi wa asilimia sawa ya 3.03 jinsi yalivyotamkwa na wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Mukuli. Isitoshe, msamiati uliotumiwa na wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Mukuli ulitokana na mbinu za uundaji wa maneno ya Sheng namna ilivyoelezwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

na Ogechi (2005). Mfano ni neno *ticha* ambalo limetokana na mbinu ya utohozi ilhali maneno *mtoi* na *piko* yametokana na mbinu ya ufupisho.

*Jedwali 2* pia linaonyesha kwamba wanafunzi wa darasa la kwanza walikuwa na asilimia ya 39.394 ya umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng jinsi ilivyorekodiwa ikitumiwa miongoni mwao darasani. Hii ilifuatiwa na umaratokezi wa asilimia 33.333 ya wanafunzi wa darasa la pili hatimaye umaratokezi wa asilimia 27.273 ya wanafunzi wa darasa la tatu.

*Jedwali 2* linaonyesha msamiati wa Sheng ambao ulikuwa na umaratokezi wa juu kimatamshi ni *ticha* (umaratokezi wa asilimia 66.667), *mtoi* (umaratokezi wa asilimia 15.152) na *piko* (umaratokezi wa asilimia 6.061). Matokeo haya yanalingana na mawazo ya Bybee (2006) anaposema kwamba, aina ya umaratokezi husaidia katika utambuzi wa mlingano kati ya miundo. Hali hii huhitajika ili kuweka wazi miundo ya maneno. Matokeo ya utafiti yamethibitisha kuwepo kwa mfanano wa matumizi kati ya miundo ya msamiati wa Sheng na matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, wanadaraja la awali walitumia neno la Sheng *ticha* kwa kufananisha maana yake na neno la Kiswahili mwalimu, neno *mtoi* (Sheng) kufananishwa na mtoto (Kiswahili) na *piko* (Sheng) kulinganishwa na pikipiki (Kiswahili).

Kwa mujibu wa mhimili wa miundo huibuka kutoka kwa matumizi, inasemekana kwamba skima huchangia katika upokezilugha kwa sababu kategoria za skima ya juu hupelekwa kwa urahisi hadi kwa faridi mpya. Kwa kufanya hivyo, skima huchangia katika kuunda kategoria za kiisimu.

Mawazo ya Tomasello (2003) yamethibitishwa na matokeo ya utafiti kwa kuwa umaratokezi wa juu ya neno *ticha*, *mtoi* na *piko* imedhihirisha kwamba hizi ni faridi mpya zinazotokana na msamiati asilia wa Kiswahili; yaani neno *ticha* limetokana na maana ya mwalimu, *mtoi* limetokana na mtoto na *piko* limetokana na pikipiki.

**Umaratokezi katika Shule ya Shalom**

Kati ya maneno kumi na tano yaliyokuwa kwenye mwongozo wa uchunzaji, maneno kumi na moja yalibainika katika matumizi ya wanadaraja la awali wakati wa kipindi cha Kiswahili.

Kwa kurejelea *Jedwali 3*, neno *ticha* limejitokeza katika matumizi ya wanadaraja la awali kwa umaratokezi wa asilimia 48.28; neno *mtoi* kwa umaratokezi wa asilimia 15.52; *piko* kwa umaratokezi wa asilimia 13.81; *tao* kwa umaratokezi wa asilimia 6.9; *kanjo* kwa umaratokezi wa asilimia 5.17 kisha maneno mengine kama *poa*, *moti*, *mandanyo*, *baro*, *pupuu* na *susuu* yalitamkwa kwa umaratokezi wa asilimia sawa ya 1.72 kila moja.

Kwa kulinganisha asilimia ya umaratokezi wa matumizi ya msamiati teule wa Sheng miongoni mwa wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Shalom, *Jedwali 3* linaonyesha kuwa, asilimia 48.28 ya umaratokezi inatokana na wanadarasa la kwanza, asilimia ya 27.59 ya wanadarasa la pili halafu asilimia 24.13 ya wanafunzi wa darasa la tatu.

**Jedwali 3: Limewasilisha msamiati teule wa Sheng kutokana na uchunzaji darasani**

| **Sheng** | **Shule** | **Shalom** | | | **Jumla** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasa** | **1** | **2** | **3** | | |
| | **Kiswahili** | | | | | |
| *Ticha* | Mwalimu | 06 | 11 | 11 | 28 | 48.28 |
| *Mtoi* | Mtoto | 05 | 02 | 02 | 09 | 15.52 |
| *Piko* | Pikipiki | 08 | - | - | 08 | 13.81 |
| *Tao* | Mjini | 04 | - | - | 04 | 6.9 |
| *Kanjo* | Askari wa baraza la mji | 03 | - | - | 03 | 5.17 |
| *Poa* | Vizuri | - | - | 01 | 01 | 1.72 |
| *Moti* | Motokaa | 01 | - | - | 01 | 1.72 |
| *Mandanyo* | Mandazi | - | 01 | - | 01 | 1.72 |
| *Baro* | Barabara | 01 | - | - | 01 | 1.72 |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

| Sheng | Shule | Shalom | | | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasa** | **1** | **2** | **3** | | |
| | **Kiswahili** | | | | | |
| *Pupuu* | Enda haja kubwa | - | 01 | - | 01 | 1.72 |
| *Susuu* | Enda haja ndogo | - | 01 | - | 01 | 1.72 |
| Jumla | | 28 | 16 | 14 | 58 | |
| % | | 48.28 | 27.59 | 24.13 | | 100 |

*Jedwali 3* linaonyesha msamiati wa Sheng ambao ulikuwa na umaratokezi wa juu kimatumizi ni *ticha* (umaratokezi wa asilimia 48.28), *mtoi* (umaratokezi wa asilimia 15.52), *piko* (umaratokezi wa asilimia 13.81), *tao* (umaratokezi wa asilimia 6.9) na *kanjo* (umaratokezi wa asilimia 5.17). Kuambatana na utafiti wa Bybee (2006), aina ya umaratokezi husaidia katika utambuzi wa mlingano kati ya miundo. Hali hii huhitajika ili kuweka wazi miundo ya maneno. Matokeo ya utafiti yamethibitisha kuwepo kwa mfanano wa matumizi kati ya miundo ya msamiati wa Sheng na ya Kiswahili katika matamshi ya wanadaraja la awali. Kwa mfano, wanadaraja la awali walitumia neno la Sheng *ticha* kwa kufananisha na maana ya neno la Kiswahili mwalimu, neno *mtoi* (Sheng) kufananishwa na mtoto (Kiswahili), *piko* (Sheng) kulinganishwa na pikipiki (Kiswahili), *tao* (Sheng) kufananishwa na mji (Kiswahili) na neno *kanjo* (Sheng) kulinganishwa na askari wa baraza la mji (Kiswahili).

**Umaratokezi katika Shule ya Idavaga**

Maneno tisa yalionekana kutumiwa na wanadaraja la awali kutokana na idadi jumla ya maneno kumi na tano ya Sheng yaliyokuwa kwenye mwongozo wa uchunzaji. Jedwali 4 linadhihirisha umaratokezi wa asilimia 46.51 ya neno *ticha* namna lilivyojitokeza katika matamshi ya wanadaraja la awali katika Shule ya Msingi ya Idavaga. Neno lililofuata lilikuwa *tao* ambalo lilitamkwa kwa umaratokezi wa asilimia 18.6.

**Jedwali 4: Umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng katika Shule ya Idavaga:**

| Sheng | Shule | Idavaga | | | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Darasa** | **1** | **2** | **3** | | |
| | **Kiswahili** | | | | | |
| *Ticha* | Mwalimu | 07 | 08 | 05 | 20 | 46.51 |
| *Tao* | Mjini | - | 05 | 03 | 08 | 18.60 |
| *Poa* | Vizuri | 04 | 01 | 01 | 06 | 13.95 |
| *Mtoi* | Mtoto | - | 03 | - | 03 | 6.97 |
| *Sonko* | Tajiri | 02 | - | - | 02 | 4.65 |
| *Bamba* | Furahisha | 01 | - | - | 01 | 2.33 |
| *Piko* | Pikipiki | - | - | 01 | 01 | 2.33 |
| *Moti* | Motokaa | - | - | 01 | 01 | 2.33 |
| *Mandanyo* | Mandazi | - | 01 | - | 01 | 2.33 |
| Jumla | | 14 | 18 | 11 | 43 | |
| % | | 32.56 | 41.86 | 25.58 | | 100 |

Neno *poa* lilirekodi umaratokezi wa asilimia 13.95; neno *mtoi* likawa na umaratokezi wa asilimia 6.97; neno *sonko* lilirekodi umaratokezi wa asilimia 4.65 kisha maneno *bamba*, *piko*, *moti* na *mandanyo* yalitamkwa kwa umaratokezi wa asilimia sawa ya 2.33 kila moja.

Kwa upande mwingine, *Jedwali 4* linaonyesha asilimia ya juu ya wanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi ya Idavaga walikuwa na umaratokezi wa juu wa matumizi ya msamiati teule wa Sheng katika matamshi yao. Wanafunzi wa darasa la kwanza walifuata kwa umaratokezi wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

asilimia 32.56 hatimaye wanafunzi wa darasa la tatu wana umaratokezi wa chini wa asilimia 25.58.

*Jedwali 4* linaonyesha msamiati wa Sheng ambao ulikuwa na umaratokezi wa juu kimatumizi ni *ticha* (umaratokezi wa asilimia 46.51), *tao* (umaratokezi wa asilimia 18.60), *poa* (umaratokezi wa asilimia 13.95), *mtoi* (umaratokezi wa asilimia 6.97), *sonko* (Sheng) na neno tajiri (umaratokezi wa asilimia 4.65). Matokeo haya yanaafikiana na hoja ya utafiti wa Bybee (2006) anaposema kwamba, aina ya marafukizi husaidia katika utambuzi wa mlingano kati ya miundo. Hali hii huhitajika ili kuweka wazi miundo ya maneno. Matokeo ya utafiti yamethibitisha kuwepo kwa mfanano wa matumizi kati ya miundo ya msamiati wa Sheng na ya Kiswahili. Kwa mfano, wanadaraja la awali walitumia neno la Sheng *ticha* kwa kufananisha na neno la Kiswahili mwalimu, neno *tao* (Sheng) kufananishwa na mji (Kiswahili), *poa* (Sheng) kulinganishwa na vizuri (Kiswahili), *mtoi* (Sheng) kufananishwa na neno mtoto (Kiswahili) na neno *sonko* (Sheng) kulinganishwa na tajiri (Kiswahili).

Utafiti ulionyesha kuwa msamiati wa Sheng ndiyo uliowakilisha umbo la kiisimu ambalo kiwango chake cha umaratokezi kiliwezesha mchakato wa upokezi wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali.

Matokeo ya utafiti yanadhihirisha namna msamiati wa Sheng unaweza kuchangia katika uundaji wa skima ya juu au ya chini. Skima ya chini ingesababisha upokezi wa kiingizi cha lugha ya Kiswahili kuwa chini ama ikiwa skima ingekuwa ya juu ingesababisha upokezi wa kiingizi cha lugha ya Kiswahili kuwa juu miongoni mwa wanadaraja la awali katika shule za msingi mjini Mbale.

Ugunduzi huu unaafikiana na hoja ya Saxton (2010) anapoeleza kwamba, uundaji skima hutokana na aina ya umaratokezi. Umaratokezi unahusu umbo la kiisimu kujitokeza mara nyingi katika kiingizi. Kwa hivyo, ni kutokana na mazoea ya kutamka maneno yanayotokana na lugha kama msimu wa Sheng ambapo uwakilishi wa kiingizi cha kiisimu huimarika kwa mtoto na hili humfanya kulitoa umbo la kiisimu kwa urahisi anapohitaji kulitumia wakati mwingine.

Kwa upande mwingine, mtaalamu katika isimu, Bybee (2006) anadahili kwamba, kuna aina mbili za umaratokezi: Umaratokezi-juu kialama na aina ya umaratokezi. Ufafanuzi wa Bybee (2006) unadhihirisha kuwa aina ya umaratokezi husababisha utambuzi wa mlingano kati ya miundo ya maneno na virai. Isitoshe, aina ya umaratokezi wa juu huupatia muundo uwezo mkubwa wa kuwakilishwa, hivyo kuufanya uwepo na kutolewa kwa matumizi muhimu. Bybee anasisitiza kwamba kategoria za skima ya juu (dhahania) huweza kusaidia katika uundaji wa faridi mpya.

Matokeo ya utafiti yanaingiliana na mawazo ya Saxton (2010) pamoja na Bybee (2006) kwa kuwa yanaonyesha umaratokezi wa msamiati wa Sheng katika matamshi ya wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale. Kwa mfano, matamshi ya neno *ticha* ambalo linaonekana kuwa na umaratokezi wa juu takriban shule zote zilizoshiriki uchunguzi huu ni ithibati kwamba neno hili limedhahanishwa kutokana na neno la Kiswahili sanifu: mwalimu. Hii ndiyo sababu inawawia vigumu wanadaraja la awali kukwepa matumizi yake wakati wa somo la Kiswahili licha ya mwalimu wao kuweka juhudi za mara kwa mara kuwarekebisha. Kwa hivyo neno *ticha* ni tokeo la aina ya umaratokezi na hii ndiyo sababu ya muundo wake kukumbukwa na kutolewa kwa urahisi na wanadaraja la awali kila wanapohitaji kulitumia darasani.

## HITIMISHO

Makala hii imetathmini umaratokezi wa msamiati teule wa Sheng katika upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali kwenye shule za msingi mjini Mbale, Kenya. Matokeo ya utafiti yameonyesha kwamba, wanafunzi wa daraja la awali wanatumia lugha ya msimu ya Sheng katika mawasiliano yao wakiwa shuleni hususan darasani. Hali hii ni thibitisho kwamba, umaarufu wa matumizi ya Sheng nje ya shule huenda umesababisha wanadaraja la awali kuamili msamiati wa Sheng aidha kwa kusudi ama bila kusudi. Vilevile, makala imeonyesha kuwa wanadaraja la awali wanapoutumia msamiati wa Sheng hasa ule ulio na umaratokezi wa juu, inaelekea huwa wanaelewa maana ya matumizi yake kwa mawasiliano. Wanadaraja la awali wanaweza kutambua msamiati wa Kiswahili unaofanana na ule wa Sheng lakini wakahiari kutumia msamiati wa Sheng badala ya msamiati wa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.578

Kiswahili. Hali hii inaingiliana na mawazo ya nadharia ya Msingi wa Matumizi (Tomasello, 2003) kwamba, kiingizi bora cha upokezilugha ni kile ambacho ni rahisi kutolewa na kutumiwa kwa sababu kinafahamika kwa urahisi na anayekitumia. Fikra hizi ni sawa na za Krashen (1981) ambaye anasema kwamba, kiingizi cha kiisimu kilicho na thamani kubwa katika upokezilugha ni ile lugha ambayo imepiga hatua zaidi katika miundo ambayo mwanafunzi wa lugha tayari amepokea. Makala hii inadhihirisha kuwa, lugha ya msimu ya Sheng ina uwezo wa kuchangia katika upokezilugha wa Kiswahili. Hii ni kwa sababu, msamiati maarufu wa Sheng ambao unatumika kwa kiwango kikubwa unaweza kuimarishwa kwa kusanifishwa kwa matumizi mapana ya kijamii. Juhudi zozote za kuififisha Sheng hazitafua dafu kwa sababu Sheng inatumia muundo wa kisarufi wa Kiswahili katika kuunda msamiati wake. Isitoshe vijana ambao ndio wengi katika jamii ya Kenya wanaendelea kupanua na kustawisha matumizi ya Sheng kufikia kiwango ambapo hata watu wa umri wote na matabaka tofauti tofauti wamelazimika kutumia Sheng kwa mawasiliano yao. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa wataalamu na wasomi wa Kiswahili hususan katika taaluma ya Sheng na upokezilugha wa Kiswahili miongoni mwa wanadaraja la awali. Kwa kuwa msamiati maarufu wa Sheng umedhihirika kimawasiliano miongoni mwa wanadaraja la awali wa shule za msingi mjini Mbale, makala hii inapendekeza kwamba msamiati huo wa Sheng unaweza kutumika shuleni na walimu kufafanua dhana changamano ambazo wanafunzi wenye mazoea ya kuwasiliana kwa Sheng hawawezi kuelewa kupitia Kiswahili au Kiingereza pekee.

## MAREJELEO


Bybee, J. (2006). Frequency of Use and the Organization of Language. Oxford: Oxford University Press.

Githinji, P. (2013). "Sheng and Language Pedagogy." Paper at Sheng Language in Kenya: Structure, Uses and Pedagogy conference, IFRA, Nairobi,

Kitula, K. & Kobia, J. (2000). Lugha kama Kitambulisho: Changamoto ya Sheng Nchini *Kenya*. http://www.njas.helsinki.fl/.../king'ei&kobia.pdf,

Kothari, C. R. (2004). Research Methodology: Methods and Techniques (2nd ed.). New Delhi: New Age International (P) Ltd., Publishers.

Krashen, S. (1981). Second Language Acquisition and Second Language Learning. New York: Pergamon Press.

Langacker, W. (1987). Foundations of Cognitive Grammar: Theoretical *Prerequisites*. Stanford, CA: Stanford University Press.

Lieven, E. & Tomasello M. (2008). Children's First Language Acquisition from a Usage-Based Perspective. In P. Robinson & N. C. Ellis (Eds), *Handbook of Cognitive Linguistics* and Second Language Acquisition (pp. 168-196). London: Routledge.

Macaro, E. (2001). Analysing Students Teachers' Codeswitching in Foreign Language Classrooms: Theories and Decision Making. *The Modern Language Journal*, 85, 531-548. http://dx.doi.org/10.1111/0026-7902.00124

Ogechi, N. O. (2005). Lexicolization in Sheng'. *Nordic Journal of African Studies*, 14(3), 334-355

Saxton, M. (2010). Child Language: Acquisition and Development. Thousand Oaks, (CA): SAGE Publications Ltd.

Tomasello, M. (2003). *Constructing a Language: A Usage – Based Theory of Language Acquisition.* Cambridge, MA: Harvad University Press.

Tomasello, M. & Stahl, D. (2004). Sampling Children's spontaneous speech: how much is enough? *Journal of Child Language*, 31, 101-121. https://doi.org/10.1017/S0305000903005944


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.